

TAMKO LA MATATIZO YA KIFEDHA KWA AJILI YA ULINZI DHIDI YA KUFUKUZWA KWENYE NYUMBA

Fomu hii anaweza kupewa mwenye nyumba kwa mkono, kwa njia ya barua ya haraka au, kama ipo, kwa kutuma nakala au picha kwa barua-pepe au ujumbe wa maandishi

Mimi, (*jina la mpangaji*) _____, ni mpangaji katika (*anwani*):

Nimeshindwa kufanya malipo inavyostahili kulingana na makubaliano ya upangaji kwa sababu nimeathiriwa na moja au zaidi ya yafuatayo tangu Machi 16, 2020:

- Kupoteza mapato ya kaya;
- Kupoteza kazi au ujira;
- Kuongezeka kwa gharama za matibabu;
- Kuongeza majukumu ya utunzaji wa watoto au majukumu ya kumtunza mtu mwenye ulemavu au mzee, majeruhi au mgonjwa;
- Kuongezeka kwa gharama za utunzaji wa watoto au kumtunza mtu mwenye ulemavu au mtu mzee, majeruhi au mgonjwa; au
- Hali nyingine ambazo zimepunguza mapato yangu au kuongeza matumizi yangu.

Msaada wowote wa umma, pamoja na bima ya ukosefu wa ajira, msaada wa ukosefu wa ajira uliosababishwa na janga, na msaada mwingine wa umma ambao nimepata mnamo au baada ya Machi 16, 2020, haukidhi kikamilifu mahitaji baada ya kupoteza mapato au kuongezeka kwa matumizi.

Ninafahamu kuwa bado nina deni la kodi yangu, ambalo linapaswa kulipwa kabla ya Februari 28, 2022.

Ninafahamu kuwa lazima nitimize majukumu mengine ambayo ninaweza kuwa nayo kwa mujibu wa makubaliano yangu ya upangaji.

Ninaapa kwamba taarifa hiyo hapo juu ni kweli kadri nijuavyo na ninavyoamini. Ninafahamu inaweza kutumika kama ushahidi mahakamani na ninaweza kuadhibiwa kwa sababu ya kusema uwongo.

_____ *Tarehe*

_____ Saini ya mpangaji (*inahitajika moja tu*)

_____ Jina (lililochapwa)